*Mulika, Na. 42 (1), 66-82*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Tathmini ya Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya Karne ya 21 Nchini Tanzania: Tija na Madhara yake

*Gervas A. Kasiga*[1]
Chuo Kikuu cha Dodoma

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.5

**Ikisiri**

Makala haya yamefanya tathmini ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Makala yamechunguza tija na madhara ya muziki huu kwa wasanii na hadhira. Vigezo vya kibiashara na kidhamira viliteuliwa kushughulikia jambo hili. Kupitia tathmini, makala yamebaini kuwa katika karne ya 21 muziki wa kizazi kipya umeweza kufanikiwa kujenga mahusiano ya kifani na wasanii wa nje ya Tanzania. Pia, imebaini kuwa muziki huu unasisitiza uwepo wa mapenzi ya kweli katika jamii, unafariji, na kutia moyo kwa waliokata tamaa. Tija nyingine za muziki wa kizazi kipya zilizobainishwa ni uongezaji wa fursa za kiajira, utoaji wa elimu, na uburudishaji. Isitoshe, makala yamebaini madhara ya muziki huu yanayotokana na utumiaji wa lugha ya ufyosi, uhamasishaji wa vitendo vya ngono, na uhamasishaji wa kutumiwa mavazi yasiyofaa kwa hadhira. Vilevile, kufifisha nafasi ya nyimbo zenye kufuata maadili ya Kitanzania kusikilizwa na hadhira nalo limebainika kuwa ni suala linaloletwa na madhara ya muziki huu. Mwisho, imependekezwa kuwa ni vema kwa nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 kuweka msisitizo zaidi katika masuala yanayoweza kujenga jamii mpya ya Kitanzania kwa namna bora.

## 1.0 Utangulizi

Muziki wa kizazi kipya ni tasnia inayokua kwa kasi nchini Tanzania. Umaarufu wake umetokana na fani na maudhui yake kugusa hisia na mitazamo ya vijana (Samwel, 2015; Kasiga, 2021; Kasiga, 2022). Kimsingi, muziki huu umetokana na muziki wa kufokafoka (*Hip Hop*) kutoka nchini Marekani (Rose, 1994; Omari, 2009; Kasiga, 2022). Kukua kwake kumeleta mitindo mbalimbali yenye asili ya Tanzania na kigeni (Kasiga, 2021). Mitindo hiyo ni kama vile *Rege, R&B, Afrobeat na Dancehall*. Isitoshe, hivi sasa kumeibuka mtindo mpya wa kisingeli ambao umechanganya mitindo ya asili ya Kitanzania kama vile taarab na dansi (Zahoro, 2018; Kasiga, 2022). Bongofleva ni lakabu maarufu ya muziki huu (Mangesho, 2003; Jilala, 2008; Omari, 2011).

Kujichomoza muziki wa kizazi kipya, kwa asilimia kubwa, kulichagizwa na mabadiliko ya kiuchumi ya kidunia (Kasiga, 2022). Mabadiliko hayo yalitokea

[1] Baruapepe: kassiga@gmail.com

mwishoni mwa miaka ya 1980 na mwanzoni mwa mwaka 1990 (Chachage, 2002; Mangesho, 2003; Kasiga, 2022). Hali kadhalika, uwepo na maendeleo yake yamechangiwa na mabadiliko ya kisiasa na tawala za dunia, maendeleo ya sayansi na teknolojia, na mabadiliko ya mfumo wa kisiasa yaliyotokea nchini Tanzania, na bara la Afrika kwa upana wake (Mamdani, 1996; Olukoshi, 2004; Kasiga, 2021).

Kupitia data za makala, imebainika kuwa kuanzia karne ya 21 muziki huu umeongeza idadi kubwa ya wasanii na washabiki wake. Jambo hili limedhihirika kupitia uchunguzi uliofanyika katika mtandao wa *YouTube* na kubaini kuwa wasikilizaji na watazamaji wengi wamekuwa wakisikiliza nyimbo hizo mitandaoni. Ilibainika kuwa nyimbo hizo zimekuwa na wasikilizaji kati ya milioni 1 hadi 60 ndani ya mtandao huo. Wengi wa washabiki wamebainika kutokea ndani ya Tanzania na nchi jirani kama vile Kenya, Rwanda, Burundi, Msumbiji, Visiwa vya Komoro na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Jambo hilo limethibitika kuupa sura ya kibiashara muziki wa kizazi kipya (Kasiga, 2022). Isitoshe, mkondo wa kibiashara umewezesha kutoa ajira kwa wasanii pamoja na wadau wengine wa muziki (Kasiga, 2022).

Zaidi ya hayo, imebainika kuwa fursa hiyo ya kiuchumi imesaidia kupunguza tatizo la ajira nchini Tanzania, hususani kwa vijana (Kasiga, 2021). Hii ni kutokana na kwamba, katika miaka ya karibuni, sekta ya sanaa nchini Tanzania imekuwa ikiingia katika sekta tatu bora zinazochangia uchumi wa Tanzania (Kasiga, 2022). Sekta hii imekuwa ikienda sambamba na sekta ya madini na utalii katika kuchochea uchumi wa nchi ya Tanzania (Kasiga, 2022). Hivyo, jambo hilo linathibitisha kuwa endapo muziki huu utawekewa mikakati bora, utakuwa sekta muhimu ya kuupandisha uchumi wa Watanzania.

Hivyo basi, kwa hali hiyo, makala haya yameona ni jambo la muhimu kujikita katika kufanya tathmini ya nyimbo za muziki huu ndani ya karne ya 21. Lengo kubwa ni kutaka kubaini tija na madhara yake kwa wasanii na hadhira. Zaidi, kupitia tathmini, mikakati bora ya kuweza kuukuza na kuuendeleza muziki wa kizazi kipya kadiri ya maadili, utamaduni, na mazingira ya Kitanzania imependekezwa.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Makala yametumia Nadharia ya Upokezi. Kimsingi, nadharia hii inajikita katika kuchagiza namna hadhira (wasomaji, wasikilizaji na watazamaji) wanavyoweza kuisoma na kuielewa kazi ya fasihi kulingana na maarifa yao ya kielimu, mazingira, wakati, pamoja na mtazamo wao wa kimaisha (Lobo, 2015). Zaidi, Nadharia ya Upokezi kwa kina inajielekeza kuchunguza mwitikio wa usomaji wa matini za kifasihi katika miktadha ya kilimbwende na kisaikolojia (Wafula na Njogu, 2007). Kupitia nadharia hii, kwa mujibu wa misingi ya kilimbwende na imani, inabainishwa kuwa utungaji na upokeaji wa kazi za sanaa (fasihi ikiwemo), kwa

kiwango kikubwa, hushirikisha hisi. Hii inamaanisha kuwa hisi ndiyo kiini cha msukumo wa kutunga kazi ya kisanaa. Hivyo basi, kwa mantiki hiyo, hata msomaji huipokea kazi ya kisanaa kwa kuzingatia mielekeo ya hisi zake binafsi (Fish, 1980). Katika uchambuzi wa data za makala haya, athari za kitajiriba, kisaikolojia, na masuala ya kijamii na kitamaduni yanayoizunguka hadhira ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania, yalizingatiwa kadiri ya mwelekeo wa waasisi wa Nadharia ya Upokezi ambao ni Stanley Fish, Jane Tompkins, na Wolfgang Iser (Anderson, 2012). Mathalani, katika uchambuzi wa data za makala, mianya iliyoachwa wazi na watunzi wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya ilipatiwa maana kupitia mitazamo ya hadhira ya muziki wa kizazi kipya pamoja na hisi za mtafiti. Hali kadhalika, kupitia mchakato wa Nadharia ya Upokezi, nyimbo za muziki wa kizazi kipya zilisikilizwa, zilitolewa tafsiri, kadiri ya ufundi wa lugha uliotumiwa na watunzi katika uwasilishaji wa kazi zao. Yote ikiwa ni kusaidia ujengaji wa hoja kuntu za makala haya.

## 3.0 Uchambuzi na Uwasilishaji wa Data za Makala

Sehemu hii imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data za makala. Uchambuzi umejikita katika kufanya tathmini ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21. Vigezo vya kibiashara na kidhamira viliteuliwa kufanyiwa tathmini. Tathmini iliyofanyika imeakisi maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza limetazama tija za muziki wa kizazi kipya kwa jamii ya Kitanzania ndani ya karne ya 21. Eneo la pili, limefanya tathmini ya madhara ya muziki wa kizazi kipya kwa jamii ya Kitanzania ndani ya karne ya 21. Mbinu za kitaamuli zimetumika katika uchambuzi wa data za makala. Kwa mantiki hiyo, tafakuri ilikuwa kiini katika kuhusisha na kutoa majawabu ya data mbalimbali zilizochunguzwa katika utafiti wa makala haya. Utafiti wa data za makala ulifanyika maktabani na uwandani. Mbinu hizi zilihusisha uchambuzi wa kina wa nyimbo na mahojiano ya uwandani. Uwandani, utafiti uliendeshwa katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma. Majiji haya yalichaguliwa kutokana na kuchagizwa na ufanyikaji wa shughuli za tasnia ya muziki pamoja na upatikanaji wa wasanii wa muziki wa kizazi kipya na hadhira yake. Njia ya mahojiano ilitumika kupata data za uwandani. Watoataarifa waligawanywa kiuwakilishi kuanzia wasanii na wasikilizaji wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Jumla ya nyimbo 30 za muziki wa kizazi kipya zilichunguzwa. Uteuzi wa nyimbo hizi ulizingatia kigezo cha kuwa zimetolewa kuanzia mwaka 2000 hadi 2023. Nyimbo, majina ya wasanii, na lakabu zao za kimuziki zimeorodheshwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 1: Orodha ya Nyimbo za Kizazi Kipya Zilizochunguzwa**

| Na. | Jina la Wimbo | Jina la Msanii Aliyeimba |
|---|---|---|
| 1 | Make Me Sing | Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) na Kiernan Jerryd Forbes (A.K.A) |
| 2 | Nana | Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) |
| 3 | African beauty | Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) |

| **Na.** | **Jina la Wimbo** | **Jina la Msanii Aliyeimba** |
|---|---|---|
| 4 | Marry you | Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) na Shaffer Chimere Smith (NeYo) |
| 5 | Ntade | Hellen George (Rubby) |
| 6 | Yalaiti | Hamis Mwinjuma (Mwana FA) na Lina Sanga |
| 7 | Juu | Juma Mussa (Jux) na Vanessa Mdee |
| 8 | Kaza Roho | Salum Nyangumwe (Golden) na Karen Garder (Malkia Karen) |
| 9 | Alele | Hellen George (Rubby) |
| 10 | Never Give Up | Rajabu Kahali (Harmonize) |
| 11 | Nenda kamwambie | Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) |
| 12 | Nikumbushe | Kevin Mbuvi Kioko (Bahati) akimshirikisha Raymond Shabani (Rayvanny) |
| 13 | Bado kidogo | Bernard Paul (Ben Paul) |
| 14 | Nisamehe | Kala Jeremiah na Aslay Isihaka Nassoro (Aslay) |
| 15 | Sina | Rajabu Kahali (Harmonize) |
| 16 | Kivuruge | Faustina Charles Mfinanga (Nandy) |
| 17 | Never Ever | Vanessa Mdee |
| 18 | Seduce Me | Ali Kiba |
| 19 | Ninogeshe | Faustina Charles Mfinanga (Nandy) |
| 20 | Salome | Nasibu Abdul (Diamond) |
| 21 | Sukari | Zuhura Othman Soud (Zuchu) |
| 22 | Kwangwaru | Rajabu Kahali (Harmonize) na Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) |
| 23 | Muhogo | Mwajuma Abdul Juma (Queen Darleen) |
| 24 | Katika | Kundi la Muziki la Navy Kenzo |
| 25 | Kainama | Rajabu Kahali (Harmonize), Damini Ebunoluwa Ogulu (Burna Boy) na Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) |
| 26 | Ndegele | Richard Martin Lusinga (Rich Mavoko) |
| 27 | Kibamia | Kundi la Muziki la Rostam na Maua Sama |
| 28 | Nyegezi | Raymond Shabani (Rayvanny) na Nasibu Abdul (Diamond Platinumz) |
| 29 | Jeraha | Abdul Kiba |
| 30 | Niue | Abdul Juma Iddi (Lavalava) |

## 3.2 Tija za Muziki wa Kizazi Kipya wa Karne ya 21 Nchini Tanzania

Katika sehemu hii tumejikita kutazama tija za muziki wa kizazi kipya kwa jamii ya karne ya 21. Makala yamechambua namna ambavyo nyimbo za muziki wa kizazi kipya zinaleta tija kwa wasanii na hadhira yake. Tija hizi zimebainishwa kwa namna mbili;tija za kibiashara na tija za kidhamira. Kimsingi, mjadala mkubwa katika sehemu hii umejengwa na hoja mbalimbali zilizotokana na mahojiano baina ya mwandishi na hadhira ya muziki huu. Hali kadhalika, hoja nyingine zimejengwa kupitia uchambuzi wa mashairi ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya uliofanyika.

Katika aya zinazofuata, vipengele sita vimebainishwa kama tija zinazotokana na muziki huu. Vipengele hivyo ni kama ifuatavyo:

### 3.2.1 Tija za Kibiashara

Kipengele hiki kimejadili tija za kibiashara zinazopatikana kupitia muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Hoja zilizojadiliwa zimehusisha ujengaji wa mahusiano ya kifani baina ya wasanii wa Kitanzania pamoja na wasanii wa nje ya Tanzania. Hoja nyingine iliyojadiliwa ni uongezaji wa fursa za ajira kupitia tasnia ya muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania.

#### 3.2.1.1 Ujengaji Mahusiano ya Kifani na Wasanii wa Nje ya Nchi

Utafiti wa makala umebaini kuwa kupitia muziki wa kizazi kipya, wasanii wa Kitanzania hupata nafasi ya kushirikiana na wasanii wa nje. Imebainika kuwa kupitia ushirikiano huo wasanii hupata wasaa wa kubadilishana ujuzi wa kitasnia na hivyo kusaidia kuboresha kazi zao. Uchunguzi wa makala umebaini kuwa jambo hili, kwa kiasi kikubwa, limekuwa likifanywa kwa juhudi binafsi za wasanii wenyewe (Kasiga, 2022). Juhudi zao zimezaa matunda kwa kuwezesha nyimbo zao ziweze kukua na kuenea, Afrika na duniani. Mfano mzuri ni msanii Diamond Platinumz ambaye amejitengenezea soko la muziki hadi nje ya mipaka ya Tanzania. Uwezo wake wa kushirikiana na wasanii mbalimbali ndani na nje ya nchi umeongeza tija za muziki wa kizazi kipya. Mathalani, amewahi kushirikiana na kundi la Navy Kenzo katika wimbo wa "Katika". Zaidi, ameshirikiana na wasanii wa nje katika nyimbo zake mbalimbali. Nyimbo hizo ni kama vile: "Make Me Sing" alioimba na msanii A.K.A kutoka Afrika Kusini, "Nana" alioimba na Mr. Flavour kutoka Nigeria, "African Beauty" alioimba na Omarion kutoka Marekani, na "Marry You" alioimba na NeYo pia kutoka nchini Marekani.

#### 3.2.1.2 Uongezaji wa Fursa za Ajira

Fursa kubwa ya vijana kujiajiri imekuwa ikitolewa na tasnia ya muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania (Kasiga, 2018). Nyimbo za muziki huu zimekuwa biashara kubwa katika soko la burudani (Kasiga, 2022). Kupitia biashara ya muziki huu, wasanii wamekuwa wakijipatia kipato kikubwa cha kuweza kujikimu kimaisha. Fedha wanayoipata kupitia muziki wamekuwa wakiiwekeza katika biashara nyingine na hivyo kuongeza nafasi zaidi za ajira kwa watu wengine, hususani vijana. Mathalani, kupitia mahojiano tuliyoyafanya msanii wa muziki wa kizazi kipya, Mtoataarifa wa Kwanza[2], anasema:

> Kwa upande wangu mimi naona muziki wa kizazi kipya umeajiri vijana wengi ambao walikuwa hawajiwezi kimaisha. Vijana hao hivi sasa wamekuwa watu wakubwa na wa kuheshimiwa katika jamii. Hili unaweza kuliona kupitia Diamond Platnumz (Nasibu Abdul). Ukimfuatilia kuanzia alipotoa wimbo wake wa mwanzo

[2] Huyu ni msanii chipukizi wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Majengo Sokoni, jijini Dodoma, Januari 13, 2021.

> wa "Nenda Kamwambie" hadi hivi sasa, utagundua kuwa tasnia ya muziki inalipa. Hili liko bayana kwa uwezo wa kipato alionao hivi sasa. Kikubwa ni wewe kama msanii una dhamira ya kiwango gani na unajituma vipi ili uyafikie mafanikio.

Mwandishi wa makala haya analiunga mkono dai hili kwani ni kweli kwamba wasaniii wengi wamepata mafanikio makubwa kupitia muziki wa kizazi kipya. Wasanii kama vile Lady Jaydee, Mr. II Sugu, Alikiba, Ommy Dimpozi, Harmonize, na kundi la Navy Kenzo wamejijengea heshima kubwa kijamii kupitia kipato chao kutokana na biashara ya muziki. Wasanii wengine kama Vanessa Mdee, Rayvanny, Jux na Diamond Platnumz ni mifano dhahiri ya wasanii waliofanikiwa kwa kiasi kikubwa kimuziki na biashara nyingine nje ya muziki. Mathalani, msanii Diamond Platinumz, licha ya kuwa na lebo ya muziki, ameweza kufungua biashara ya kituo cha televisheni ambayo inaajiri vijana wengi wenye vipaji vya muziki na hata wale walio nje ya fani ya muziki.

**3.2.2 Tija za Kidhamira**

Kipengele hiki kimejadili tija za kidhamira za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Hoja zilizojadiliwa zimehusisha usisitizaji wa mapenzi ya kweli na uvumilivu, pamoja na ufariji na utiaji moyo. Hoja nyingine zilizojadiliwa zimehusisha utoaji wa elimu na uburudishaji.

**3.2.2.1 Usisitizaji wa Mapenzi ya Kweli na Uvumilivu**

Kimsingi, muziki wa kizazi kipya, licha ya kujenga uhusiano baina ya wasanii, bado unabeba ujumbe wenye kusisitiza mapenzi ya dhati. Mathalani, kupitia data za makala haya, ilithibitika kuwa baadhi ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya zina ujumbe wa kutia moyo na unaosisitiza mtu kuwa na uvumilivu katika mahusiano. Kwa mfano, jambo hilo linathibika kupitia wimbo wa "Ntade" wa msanii Ruby. Wimbo huu unaelezea umuhimu wa kuwa na mapenzi ya dhati na uvumilivu katika mahusiano. Jambo lingine linalosisitizwa katika wimbo huo ni suala la kuridhika katika mahusiano hata kama hali ya kiuchumi ya mwenza wako ni ya chini. Nyimbo nyingine ambazo zilibainika kuwa na maudhui yanayosisitiza mapenzi ya dhati ni "Yalaiti" wa Mwana FA akimshirikisha Linah, "Juu" wa Jux pamoja na Vanessa Mdee, na wimbo wa "Kaza Roho" wa msanii Golden akimshirikisha Malkia Karen.

**3.2.2.2 Ufariji na Utiaji Moyo**

Tija nyingine ya muziki wa kizazi kipya iliyobainika ni kuwa muziki huu umebeba ujumbe wa kufariji na kutia moyo. Hii ni kutokana na kwamba wasanii huimba mambo halisi ambayo yanatokea katika jamii zao. Katika mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na watoataarifa, kati ya watoataarifa kumi waliohojiwa, saba kati yao walishadidia hoja hii. Watoataarifa watano wa kike kati ya saba walidai kuwa nyimbo za muziki wa kizazi kipya ni moja kati ya nyimbo wanazopenda kusikiliza mara nyingi. Wanabainisha kuwa usikilizaji wao wa muziki huu hushamiri pindi

wanapopitia wakati mgumu wa mahusiano ya kimapenzi. Katika kuthibitisha jambo hilo, Mtoataarifa wa Pili[3] anasema:

> Kuna baadhi ya nyimbo za muziki ukizisikiliza unaweza ukahisi msanii alikutungia. Hii ni kutokana na hali halisi ya maisha unayokuwa unaipitia kwa wakati huo. Mathalani, mimi napenda sana kusikiliza wimbo wa "Alele" wa msanii Ruby. Ninaupenda kwa sababu kipindi wimbo huu unatoka nilikuwa nimeachana na mpenzi wangu. Kwa hiyo, muda mwingi nilikuwa ninausikiliza wimbo huu kujifariji. Nilikuwa nikiusikiliza wimbo huu kwa kuamini hata yeye (mpenzi wangu tuliyeachana) yatamkuta na atapitia kipindi kigumu kama nilichokuwa nacho… (Ufafanuzi katika mabano ni wa mtafiti)

Maoni hayo ya mtoataarifa yanathibitisha bayana kuwa nyimbo za muziki wa kizazi kipya zina umuhimu mkubwa kwa jamii. Nyimbo hizi zinaweza kumbadilisha mtu fikra, kumtia moyo, pamoja na kumfanya ajione wa thamani. Isitoshe, licha ya muziki huu wa kizazi kipya kufariji na kutia moyo katika suala la mahusiano ya kimapenzi, bado zina nguvu kubwa ya kutia moyo katika maisha ya kawaida. Mathalani, makala yalibaini katika wimbo wa "Never Give Up" wa msanii Harmonize umejikita kuhamasisha vijana kutokata tamaa katika kufanya kazi na kujiletea maendeleo. Hali kadhalika, kupitia Nadharia ya Upokezi, ilibainika kuwa maoni ya mtoataarifa yalijikita katika hadhira ashiria. Kulingana na mawazo ya mwanazuoni Iser (1980) kuhusu Nadharia ya Upokezi, ilithibitika kuwa mtoataarifa ni hadhira ashiria kwa sababu ya kubeba vigezo na sifa ya kuona, kusikia, na kugusa. Kwa hali hiyo, maoni yake yalikuwa faafu kutokana na kubainisha mguso wake wa kihisia uliobebwa na uzoefu wake mpana kuhusu usikilizaji wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya.

#### 3.2.2.3 Utoaji wa Elimu

Muziki wa kizazi kipya umekuwa ukitoa mafunzo mbalimbali ya kimaisha kupitia mashairi ya nyimbo zake. Jumbe zinazobebwa katika nyimbo za kizazi kipya zimekuwa zikiiasa jamii kuachana na ngono zembe, pamoja na kukemea rushwa na ufisadi. Zaidi, zimekuwa zikihamasisha uongozi bora, umoja na mshikamano, amani, na maadili katika jamii. Kimsingi, wasanii wamekuwa wakitoa tungo zinazoakisi masuala mbalimbali yaliyopo katika mazingira halisi wanayoishi. Akilitolea maoni jambo hili, Mtoataarifa wa Tatu[4] anasema;

> Mimi napenda sana kusikiliza nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa sababu kuna jumbe za kimaisha nazipata katika nyimbo hizo. Katika maisha yangu, haiwezi siku kupita bila mimi kusikiliza

[3] Huyu ni shabiki wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Area C jijini Dodoma, Januari 13, 2021.
[4] Huyu ni shabiki wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Nkuhungu, jijini Dodoma, Januari 20, 2020.

> wimbo wa kizazi kipya. Simu yangu imejaa nyimbo kiasi kwamba hata nikitaka kuongeza nyingine ni lazima nifute zile za zamani kidogo ili niweke mpya. Nyimbo nyingi ninazozisikiliza ni zile zenye kutoa hamasa ya kufanya mambo bora katika maisha…

Maoni hayo ya mtoataarifa yanathibitisha kuwa, nyimbo za muziki wa kizazi kipya zina dhima kubwa ya kuielimisha jamii. Makala yamebaini nyimbo kadhaa zilizobeba jumbe za kuelimisha. Nyimbo hizo ni kama vile "Nikumbushe" wa msanii Bahati akimshirikisha Rayvanny, "Bado kidogo" ulioimbwa na Ben Paul, wimbo wa "Nisamehe" ulioimbwa na Kala Jeremiah akimshirikisha Aslay. Vilevile, kupitia mashairi ya wimbo wa "Sina" wa msanii Harmonize, ilibainika wazi kuwa msanii alikuwa akiiasa jamii hususani vijana kuhusu suala la kujisahau baada ya kupata mafanikio kidogo. Kujisahau huko hufanya washindwe kutafakari maisha ya mbeleni na hatimaye kuishia katika majuto.

#### 3.2.2.4 Uburudishaji

Kupitia makala haya tulibaini kuwa muziki wa kizazi kipya una tija kubwa kiuburudishaji. Nyimbo za muziki huu zimekuwa zikitoa burudani kubwa kwa hadhira yake ambayo ni Watanzania na nchi jirani zinazozungumza lugha ya Kiswahili. Muziki wa kizazi kipya umekuwa ukipigwa katika kumbi za starehe, kwenye sherehe, na matamasha tofauti ya kimuziki. Katika maeneo yote hayo ya burudani, muziki huu umekuwa ukibeba dhima kubwa ya kuburudisha hadhira yake. Zaidi, muziki huu umekuwa ukichezwa redioni na katika vituo vya runinga ili kuvutia wasikilizaji na watazamaji. Vilevile, ilibainika kuwa muziki wa kizazi kipya umekuwa ukisikilizwa pindi vijana wakiwa nyumbani na pindi wakiwa katika shughuli ndogondogo za kiuchumi hususani kwa waendesha usafiri wa bodaboda. Isitoshe, ilibainika kuwa vijana wamekuwa wakisikiliza muziki wa kizazi kipya wakiwa wamejipumzisha. Akitoa maoni kuhusu jambo hili, Mtoataarifa wa Nne[5], mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma anasema:

> Mimi kwa siku naweza nisitoke ndani nisikilize tu nyimbo za kizazi kipya. Ninapenda sana muziki. Kwa mfano, nikiwa na mawazo labda nimezinguana (nimekosana) na mpenzi wangu nikisiliza tu zile nyimbo ninazozipenda nasahau kabisa kama tumegombana. Nishazoea kila ninapoenda niko na *headphone* (kifaa cha kusikiza muziki masikioni) kiasi kwamba nahisi muda mwingine ngoma za masikio zinataka kupasuka… (Ufafanuzi katika mabano ni wa mwandishi wa makala)

Nyimbo za "Never ever" wa msanii Vanessa Mdee, "Seduce Me" wa msanii Ali Kiba, "Ninogeshe" na "Kivuruge" wa msanii Nandy, na "Nana" wa msanii Diamond Platinumz zimebainika kuteka masikio ya hadhira ya muziki huu. Nyimbo

[5] Huyu ni shabiki wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma, jijini Dodoma, Januari 19, 2021.

nyingine zilizobainika kuwa na wasikilizaji wengi mitandaoni ni kama vile, “Salome” wa Diamond Platinumz akimshirikisha Rayvanny, “Sukari” wa msanii Zuchu, na “Kwangwaru” wa msanii Harmonize. Hivyo basi, ni bayana kwamba muziki wa kizazi kipya una maudhui yenye ujumbe wa kuburudisha hadhira yake. Licha ya hadhira kupata jumbe mbalimbali za kuelimisha kutoka katika mashairi ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya, bado hupata nafasi ya kukonga nyoyo kwa burudani anayoipata ndani yake.

### 3.3 Madhara ya Muziki wa Kizazi Kipya wa Karne ya 21

Katika sehemu hii, tumejikita kutazama madhara ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa jamii ya karne ya 21. Katika eneo hili, makala yamechambua na kubainisha namna ambavyo nyimbo za muziki wa kizazi kipya zimebeba maudhui ambayo yana ukakasi uletao madhara kwa hadhira au jamii kwa upana wake. Nyimbo sita za muziki wa kizazi kipya zimechambuliwa na kufanyiwa tathmini. Nyimbo hizo ni “Muhogo” wa msanii Queen Darleen, “Katika” wa kundi la Navy Kenzo wakishirikiana na msanii Diamond Platnumz, “Kainama” wa Harmonize akishirikiana na Burna Boy pamoja na Diamond, na “Ndegele” wa msanii Rich Mavoko. Nyingine ni “Kibamia” wa kundi la Rostam wakishirikiana na Maua Sama, “Nyegezi” wa msanii Rayvanny akimshikirisha Diamond Platnumz, “Jeraha” wa msanii Abdul Kiba, pamoja na wimbo wa “Niuwe” wa msanii Lavalava. Katika vipengele vinavyofuatia tumejadili kwa kina madhara yanayoletwa na nyimbo hizo kijamii.

#### 3.3.1 Madhara ya Kibiashara

Kipengele hiki kimejadili madhara ya kibiashara yanayojitokeza kupitia muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Hoja moja imejadili madhara haya. Hoja hiyo imebainisha kutopatiwa nafasi kwa nyimbo za kuelimisha katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii yenye mrengo wa kutoa burudani ya muziki huu.

##### 3.3.1.1 Kutopatiwa Nafasi Nyimbo za Kuelimisha

Uchunguzi wa data za makala haya ulibaini kuwa, nyimbo nyingi kugubikwa na maudhui yasiyofaa kumesababisha nyimbo zenye maadili kutopatiwa nafasi. Imebainika kuwa jambo hili limesababishwa na nyimbo na video nyingi zilizosheheni mashairi yenye lugha ya ufyosi na mavazi yaliyo nje na utamaduni wa Kitanzania ndizo zinapendwa sokoni (Kasiga, 2022). Hivyo, jambo hili limefanya kila msanii anayechipukia kufuata mkondo huo na hivyo kuzipa taswira mbaya nyimbo na video za muziki wa kizazi kipya. Isitoshe, hali hiyo imezidi kuleta athari kwa muktadha wa madhara kwa hadhira yake hasa vijana.

Makala yalibaini kuwa vijana wengi wa Kitanzania ni wapenzi wakubwa wa kusikiliza na kutazama video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya zenye jumbe zinazohusu vitendo vya ngono. Ithibati hii imetokana na kubainika kwa idadi kubwa ya watazamaji wa nyimbo zenye maudhui ya ngono katika akaunti za wasanii wa kizazi kipya katika mtandao wa *YouTube*. Katika uchunguzi, wimbo wa “Kainama”

ulibainika kusikilizwa na kutazamwa na watu milioni 29. Wakati wimbo wa "Nyegezi' ukiwa umesikilizwa na kutazamwa na watu milioni 64[6]. Jambo hili limebainika kufifisha nyimbo zenye jumbe za mahusiano au kutoa nasaha kwa jamii kufanya mambo mema kutopata nafasi ya kusikilizwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Hali hiyo imeanza kuwasukuma hata wasanii waliojikita katika nyimbo zisizo na lugha ya ufyosi kuanza kuandika nyimbo zenye dhima ya kuhamasisha vitendo vya ngono. Yote hiyo ni kwa ajili ya wao kupata nafasi ya kusikilizwa katika soko la muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania. Kwa mfano, wimbo wa "Jeraha" wa Abdul Kiba, ambao kupitia uchambuzi wetu tulibaini kuwa una maudhui ya mahusiano mema, unakosa nafasi katika soko la muziki wa Kitanzania. Wimbo huo umetumia namna bora ya kutoa ujumbe kupitia lugha ya Kiswahili. Mathalani, katika ubeti wa kwanza msanii anaeleza:

> "Uwoowoo! uwoouwoo! wowoooo!
> Mwenzako sijaumbwa kuchukia,
> Ndo' maana niko *fair* (niko na usawa),
> Tumeachana hilo najua,
> Ila sichoki cha kukusalimia,
> Ni salama tu usihisi,
> Labda najipendekeza,
> Najua kuwa wewe sio wangu,
> Umeshapata wa kukutuliza,
> Leo nimepita mahali,
> Nimekuta vitu uvipendavyo…."
> (Ufafanuzi katika mabano ni wa mwandishi wa makala)

Ilibainika kuwa mashairi ya wimbo huo yanaelimisha. Vilevile, ilithibitika kuwa wimbo huu haujatumia lugha yenye ukakasi au kuwa na matusi. Hata hivyo, kupitia utafiti uliofanyika, wahojiwa tisa kati ya kumi walibainika kutoufahamu wimbo huo. Hivyo basi, jambo hilo linathibitisha kuwa asilimia kubwa ya hadhira ya muziki wa kizazi kipya hususani vijana wamejikita zaidi katika nyimbo na video za muziki wa kizazi kipya zinazobeba maudhui yaliyo nje ya maadili na utamaduni wa Kitanzania.

### 3.3.1 Madhara ya Kidhamira

Kipengele hiki kimejadili madhara ya kidhamira yanayoletwa na muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Hoja zilizojadiliwa kuhusu kubainisha madhara hayo zimehusisha utumiaji wa lugha ya ufyosi, uhamasishaji wa vitendo vya ngono, pamoja na uhamasishaji wa mavazi yasiyo na maadili.

#### 3.3.3.1 Lugha ya Ufyosi

Katika uchambuzi wetu wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21, tulibaini kuwa nyimbo hizo zina lugha ya ufyosi. Isitoshe, mashairi ya nyimbo hizo yalibainika kuwa na maneno ya wazi yanayoashiria vitendo vya ngono. Zaidi,

[6] Data hizi zimechukuliwa katika Mtandao wa Kijamii wa *YouTube*, Oktoba 05, 2023.

makala yalibaini kuwa nyimbo nyingi zenye kuhamasisha matumizi ya lugha za matusi. Matusi hayo yamekuwa katika matumizi ya kawaida kwa vijana. Hii ni kwa hoja ya kuwa vijana ni wapenzi wakubwa wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya hivyo wamekuwa wakiakisi yale wanayomulikwa nayo kupitia muziki. Lugha ya matusi ilibainika kupitia wimbo wa *"Kibamia"* ulioimbwa na kundi la Rostam wakishirikiana na Maua Sama. Makala yamebaini pia kuwa wasanii wametumia lugha ya ufyosi katika maudhui ya wimbo huu kupitia kiitikio cha wimbo huu ambapo Maua Sama anasema:

> "Nimpende nani kati ya Roma au Stamina
> Ooooh Ooooh,
> Huwa kwamba kule eee,
> Wananichanganya *like* (kama),
> Oooooh uwooo,
> Nani anafaaaa,
> Na kwenye kitanda,
> Atanipa rahaaa!
> Ooooh yeeyiii!
> Sitaki Kibamiaaaeeeh,
> Mwanaume mashinee yeeeh,
> Ooooh yeeeh yeeh…" (Ufafanuzi wa katika mabano ni wa mtafiti)

Kimsingi, kupitia uchambuzi wetu na kwa kuongozwa na Nadharia ya Upokezi, ilibainika kuwa kuwa neno "kibamia", ambalo kiuhalisia linabeba dhana ya aina ya mboga ya majani, hapa lilitumika kinyume na maana iliyokusudiwa. Katika wimbo huu neno hili lilitumika kubainisha mwanamume mwenye umbile dogo la uume. Zaidi, kupitia wahojiwa wa makala, walithibitisha kuwa neno hilo kwa kipindi hiki ni msamiati wa kawaida kwa vijana. Wimbo mwingine ambao ulibainika kusheheni lugha ya ufyosi ni wimbo "Nyegezi" wa msanii Rayvanny akishirikiana na msanii Diamond Platinumz. Katika ubeti wa kwanza wa wimbo huo, Rayvanny anasema;

> "Eee nyege nyege!
> Kwetu Mwanza Nyegezi!
> Mhhhh! Nyege Nyege!
> Nishushe Mwanza Nyegezi x2
> Oyaa *whine your waist* (kata kiuno)
> Njoo unipatie komandoo
> Nikupe cha mkwezi!
> Kwa miuno ya Taikwando (mchezo wa kimapigano wenye asili ya Korea)
> Asa chekelee mwendo wa kandanda!
> Ndani ya msambwanda!
> Saa nisogezee!
> Leta msambwanda,
> Nikazie nganganga!
> Chiiiii! Ananivuta ghetoo!
> Nkapige bundukii eeh bunduki!
> Ila naogopa sentroo!

Michezo ya Amber Rutty! Amber Rutty!
(Ufafanuzi wa katika mabano ni wa mtafiti)

Ilibainika kuwa katika wimbo huu, msanii ametumia neno "Nyegezi" bila kubeba dhana ya msingi kumaanisha sehemu ya Jiji la Mwanza. Kiuhalisia, katika wimbo huu wasanii wamelitumia kuliimba kwa kulikata-kata kuashiria dhana ya ashki ya kujamiiana. Pia, msanii anaposema "Nikupe cha Mkwezi" ilibainika kuwa anamaanisha mshindo mmoja wa mwanamume autoao kwa mwanamke wakati wa tendo la kujamiiana. Vilevile, dhana ya "msambwanda" iliyotumika katika wimbo huu ilibainika kumaanisha mwanamke mwenye makalio makubwa. Isitoshe, neno bunduki, ambalo lina maana ya silaha inayotumika vitani, katika kauli, "Ananivuta ghetto nikapige bunduki eeeh bunduki", limetumika kumaanisha sehemu za siri za mwanamume. Aidha, msanii anaposema "michezo ya Amber Rutty" anamaanisha vitendo vya kufanya mapenzi kinyume cha maumbile kama ilivyokuwa imeakisiwa kutokana na uvujaji wa video ya matendo ya ngono ya msanii Nasma Abdul (Amber Rutty) iliyomuonesha akifanya vitendo hivyo. Kwa hali hiyo, ni dhahiri kuwa katika wimbo huu, msanii alitumia jina la "Nyegezi' kuficha dhana za matusi alizotaka kuzizungumzia kwenye wimbo wake. Kupitia uchambuzi wa data za makala ilithibitika kuwa wimbo huu haukubeba dhana yoyote inayojiegemeza katika kitongoji cha Nyegezi cha jijini Mwanza nchini Tanzania.

Hali kadhalika, kupitia Nadharia ya Upokezi, ujazaji wa maana iliyoachwa wazi na mtunzi wa wimbo uliotafitiwa ilifanikiwa kupitia uhusishaji wa yaliyopita na yaliyopo ili kutoa tafsiri ya maana inayofaa zaidi. Aidha, kufikiwa kwa mahitimisho hayo kulitokana na hatua za usikilizaji wa mara kwa mara na wa kina wa wimbo husika, pamoja na ujengaji wa dhana kutokana na uzoefu wa misemo ya kijamii hususani kwa vijana. Njia hiyo ilitusaidia kuipata maana fiche kutoka kwenye muktadha uliotumika katika nyimbo husika za muziki wa kizazi kipya zilizoteuliwa katika utafiti wa makala.

#### 3.3.3.2 Uhamasishaji wa Vitendo vya Ngono

Uchambuzi wa data za makala uligundua kuwa zipo nyimbo nyingi ambazo zinahamasisha vitendo vya ngono. Hili lilibainika kutokana na nyimbo hizo kuwa na jumbe za kuishajiisha hadhira yake kufanya ngono. Hatari zaidi, ngono ambayo imekuwa ikipigiwa chapuo na wasanii wa nyimbo za kizazi kipya ni ngono isiyo salama. Katika nyimbo hizo, ngono zembe imekuwa ikihamasishwa pasi na kujali uwepo wa magonjwa hatari ya kuambukizwa kwa njia ya ngono kama vile UKIMWI, kaswende, na kisonono.

Kupitia uchunguzi huu, ilibainika kuwa nyimbo hizi zimekuwa zikihamasisha vijana ambao hawajaoa wafanye ngono na wapenzi waliowazidi kiumri. Isitoshe, ilibainika kuwa hamasa hii ina mchango kubwa kwa maambukizi ya magonjwa ya zinaa kwa rika la vijana. Moja kati ya wimbo uliobainika kuwa na maudhui yanayohusisha vitendo vya ngono ni wimbo wa "Ndegele" wa msanii Rich

Mavoko. Mwandishi alibaini kuwa wimbo huu umesheheni maudhui yenye kuihamasisha hadhira kushiriki vitendo vya ngono. Katika ubeti wa pili wa wimbo huu msanii anasema:

> "She makes me koroo
> Yoo mama yoo!
> Na bodii na lelioo!
> Stimu za ugoroo!
> Ukimtazamaa ananyonga,
> Na land oooh!
> Agwelina Agwelina,
> Umenibariki kimoko!!
> Agwelina Agwelina
> Kamusuku kamusoko!
> Una bodii badii,
> Una wadrive madingi,
> Hilo bodi bodi,
> Shepu kama shangingi,
> Nipe mpaka kuchukuchu,
> Ndegele nilambe nyao mpaka chuchu,
> Ndegelee njoo ushike na mututu,
> Ndegele nisugue mpaka itoke kutu,
> Ndegele! Ndegele! Kataa!
> Ndegele! Ongeza mizuka!
> Ndegele! Jipinde binuka…"

Kupitia ubeti huu, ilibainika kuwa msanii alikuwa akichochea vitendo vya ngono kupitia wimbo huo. Kwa mfano, msanii anaeleza kuwa Agwelina ana mwili mzuri unaowachanganya watu wazima. Zaidi, anamwambia kuwa aje ashike mtutu (sehemu za uzazi za kiume) na aizisugue hadi zitoe kutu. Kwa hali hiyo, ukiutazama ubeti huo utaona kuwa vitendo vya ngono isiyo salama imehamasishwa kwa kiasi kikubwa kupitia wimbo huo.

Fauka ya hayo, uchunguzi wa makala ulibaini beti zingine zinayochochea vitendo vya ngono na uasherati zinazopatikana katika wimbo wa "Muhogo" wa msanii Queen Darleen. Hili lilibainika katika ubeti wa tatu wa wimbo huo ambapo msanii anasema;

> **Kiitikio**
> Asubuhi na muhogo
> Oyeeeah!
> Mchana kutwa na muhogo,
> Oyeeah!
> Usiku pia na muhogo,
> Oyeeeeah!
> Kiukweli napenda pendaa! X 2
> **Ubeti wa tatu**
> Sitaki unibanie banie,

Wala kunikataza kataza!
Napenda nishikilie,
Chachandu kupakaza pakaza,
Nikila lazima nilie,
Sipendi kunyamaza nyamaza!
Muhogo kiboko ya mie,
Kizungu ni kasava kasava..."

Katika wimbo huu, msanii ametumia neno "muhogo" ambalo maana yake ya msingi ni aina ya chakula jamii ya wanga. Hata hivyo, katika wimbo huu neno hili lililobainika kubeba maana ya ziada ya sehemu za siri za mwanamume. Jambo hili lilibainika kupitia uchambuzi wetu kutokana na ujumbe mkubwa wa wimbo huu kusisitiza ufanyaji wa ngono. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Upokezi, hususani katika ujazaji wa maana iliyoachwa na mtunzi, jambo hili lilithibitika kutokana na msisitizo wa msanii anaposema "sitaki unibanie banie", "napenda nishikilie', "nikila lazima nilie", na "muhogo kiboko ya mie". Kimsingi, beti za wimbo huu zilibainika kuwahamasisha watoto wa kike kushiriki ngono. Katika beti zinazofuatia za wimbo huu ilibainika kuwa msanii alikuwa akiwahimiza watoto wa kike kujituma zaidi katika vitendo ya kingono kwani kunaweza kuwaletea kipato na maendeleo. Kulithibitisha hili msanii anasema:

Kadii, garii, nyumba kalii daily party (kila siku shehere)!
Kwa sababu ya muhogooo!
Yani mwali mtamu,
Asali achali hatari! Hatarii!
Nikilaga muhogo!!
Walivyo wadogo,
Eti nao wanajiita wanadangaa!
Wanakula mihogo,
Hawamiliki hata vitanda..."
(Ufafanuzi wa katika mabano ni wa mwandishi wa makala)

Ujumbe unaopatikana katika ubeti huu unathibitisha bayana kwamba, "muhogo" unaozungumziwa hapa sio aina ya muhogo ule wa chakula. Hii ni kwa sababu, katika hali ya kawaida, mtu hawezi kununua gari au kujenga nyumba kwa kula muhogo tu. Hali hiyo, inathibitisha wazi kwamba msanii kupitia mashairi ya wimbo wake anaihamasisha hadhira yake hususani mabinti waingie katika vitendo vya ngono kama biashara ya kujiletea kipato na maendeleo katika maisha.

#### 3.3.3.3 Uhamasishaji wa Mavazi yasiyo na Maadili

Kupitia uchambuzi wa data za makala, tulibaini kuwa zipo baadhi ya nyimbo ambazo video zake zimesheheni mavazi yasiyofaa kwa maadili ya Kitanzania. Mavazi hayo yamekuwa yakivaliwa na wasanii katika video za nyimbo hizo. Kutokana na nyimbo hizo kuonekana katika mitandao ya kijamii, imekuwa vigumu kwa wazazi na wakati mwingine serikali kuzuia video hizo zisiwafikie vijana.

Hadhira kubwa ya vijana huiga mavazi hayo wanayoyaona katika video na kuyatumia katika maisha yao ya kila siku.

Utafiti umebaini kuwa mavazi yaliyo kinyume na maadili ya Kitanzania kuwa katika video ya "Katika" ya kundi la Navy Kenzo wakimshirikisha msanii Diamond Platinumz. Katika video ya wimbo huo, wasanii wa kiume walionekana kusuka mitindo ya kike pamoja na kuvaa hereni. Hata hivyo, jambo hilo kwa mazingira na maisha ya Kitanzania huonekana kuwa si jambo lenye kufaa. Pia, kupitia video hii, wasichana wameonekana kuvaa mavazi ambayo yaliacha wazi sehemu kubwa ya miili yao. Vilevile, katika wimbo wa "Kainama" wa msanii Harmonize akishirikiana na wasanii Diamond na Burna Boy, tulibaini matendo yaliyo kinyume na jamii ya Kitanzania yakifanyika katika video hiyo. Kufanyika matendo hayo kunachagizwa na uvaaji ulio kinyume na maadili.

Katika video za nyimbo za "Katika" na "Kainama" zilizotafitiwa, ilibainika kusheheni kwa matendo yanayoonesha kumdhalilisha mwanamke. Katika video ya "Kainama" mwanamke alibainika kuchorwa kama chombo cha starehe. Ndani ya video hiyo msanii Harmonize anaonekana akiwa amezungukwa na wanawake wasio na mavazi ya heshima huku wakimpapasa mwili wake. Katika video hiyo, Harmonize anaonekana akiwa kifua wazi huku akitumia mikono yake kuwashikashika wanawake hao katika maeneo tofauti ya miili yao. Vilevile, ilibainika kwamba wimbi kubwa la vijana kuiga mavazi yasiyo na staha huchochewa zaidi na mambo wanayoyaona kupitia video za nyimbo za kizazi kipya wanazozitazama kupitia televisheni na mitandao ya kijamii.

## 4.0 Mapendekezo

Kupitia utafiti uliofanyika kupitia makala haya, changamoto kadhaa zimebainishwa na kujadiliwa katika aya zilizotangulia. Aidha, kupitia data za makala, imebainishwa kuwa changamoto hizo zimesukuma kutokea kwa madhara yanayochochewa na nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Hivyo, katika jitihada za kupunguza makali ya madhara hayo, makala yanaona kuna haja ya kutia mkazo katika ubunifu ndani ya nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kimsingi, inapendekezwa kuwa wasanii na waandaaji wa kazi za muziki waongeze ubunifu katika hatua zote za usanaji wa sanaa zao. Fauka ya hayo, makala yanapendekeza kuwa kuwe na kauli moja ya watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kauli hiyo ijielekeze katika mchakato wa kuchukua mitindo ya sanaa za Kitanzania katika utengenezaji wa ala na midundo. Ni imani yetu kuwa, mabadiliko makubwa ya kitasnia yatakuwepo kupitia watayarishaji wa muziki, hususani katika kujenga namna bora ya sanaa ya muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania. Ubunifu huu ukiongezwa na vyombo vya habari vikiupa nafasi, bila shaka nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania zinaweza kuvuta mashabiki wengi katika muziki wao. Kuvutwa huku kwa mashabiki kutatokana na kuona kuwa muziki wao umewakilisha mambo yanayoigusa jamii yao kwa kiasi kikubwa.

**5.0 Hitimisho**

Makala haya yalizamia kufanya tathmini ya muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 nchini Tanzania. Katika kutathmini, makala yalijikita kutazama tija na madhara ya muziki huu kwa hadhira yake. Makala yamebaini kuwa muziki huu una tija na madhara kwa jamii ya Kitanzania. Katika tija, utafiti umebaini kuwa muziki huu una nafasi kubwa katika ujengaji wa mahusiano ya kifani na wasanii wa nje ya Tanzania, una sisitiza uwepo wa mapenzi ya kweli katika jamii, na unafariji na kutia moyo. Mengine yaliyobainishwa kama tija za muziki huu ni uongezaji wa fursa za kiajira, utoaji wa elimu, na uburudishaji. Isitoshe, makala yamebainisha kuwa madhara ya muziki huu yanatokana na utumiaji wa lugha ya ufyosi, uhamasishaji wa vitendo vya ngono, na uhamasishaji wa kutumiwa mavazi yasiyofaa kwa hadhira. Kupunguza nafasi ya nyimbo zenye kufuata maadili ya Kitanzania kusikilizwa na hadhira nalo limebainika kama suala linalotokana na madhara ya muziki huu kwa jamii. Mwisho, tunaona ni vyema kwa nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa karne ya 21 kuweka msisitizo zaidi katika masuala yanayoweza kujenga jamii mpya ya Kitanzania kwa namna bora.

**6.0 Marejeleo**

Anderson, M. (2012) *Reader-Response Theories and Life Narratives*. Alberta: Athabasca University.

Chachage, C.S.L. (2002) Ndani ya Bongo: Utamaduni na Migogoro ya Utamaduni. *Paper presented at the Tenth Conference on the Political Environment in Tanzania*, 17th – 18th September, Dar es Salaam.

Fish, S. (1980) *How to Recognize a Poem When You See One*. *Is There a Text in this Class?The Authority of Interpretive Communities*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Iser. W (1980) *The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response*. Baltimore: Johns HopkinsUniversity Press.

Jilala, H. (2008) *The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meaning and Messages in New Generation Songs in Tanzania*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria, Dar es Salaam.

Kasiga, G.A. (2022) *Tathimini ya U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili nchini Tanzania*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kasiga, G.A. (2021) "Athari za U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania". *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS*), Juz. Na. 7 (1): 118-135.

Kasiga, G.A. (2019) "*Mwanzo na Mdhihiriko wa U-Nigeria katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania*". Katika A.S. Ponera na Z.A. Badru (Wah). *Koja la Taaluma za Insia*: *Kwa Heshima ya Profesa Joshua Madumulla*. Dar es Salaam: Karljamer Publisher Limited. Kur. 663-680.

Kasiga, G.A. (2018) "U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania". *Mulika*, Juz. Na. 37: 72-84.

Lobo, A. G. (2015) "Reader-Response Theory: A Path Towards Wolfgang Iser". *Letras*, Juz. Na. 54: 13-30.

Olukoshi, A. (2004) "Changing Patterns of Politics in Africa". *Cadernos de Estudos Africanos*, Juz. Na. 6: 15-38.

Mamdani, M. (1996) *Citizen and the Subject: Contemporary Africa and the Lecacy of Colonialism*. Princeton: Princeton University Press.

Mangesho, P. (2003) *Global Cultural Trends*, *The Case of Hip-Hop Music in Dar es Salaam*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mrikaria, S. E. (2007) "Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya". *Swahili Forum*. Juz. Na. 14: 197-206.

Omari, S. (2009) *Tanzania Hip Hop Poetry as Popular Literature*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Omari, S. (2011) "Call me Top in Dar: The Role of Pseudonyms in Bongo Fleva Music". *Swahili Forum*, Juz. Na. 18, 69-66.

Samwel, M. (2015) *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: MVP.

Rose, T. (1994) *Black Noise: Rap Music and Black Culture in Contemporary America*. Middletown. Wesleyan University Press.

Wafula, R. M., na Njogu K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Zahoro, S. (2018) *Vionjo vya Fasihi ya Kisasa ya Kiswahili katika Nyimbo Teule za Singeli*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.